**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

Simu Nambari: 027-2645186,
Nukushi: 027-2647885
Barua Pepe: rbctanga@pccb.go.tz

BARABARA RA YA BOMBO HOSPITALI
S.L.P. 1953,
21105 TANGA

## TAARIFA KWA UMMA

## UTENDAJI KAZI WA TAKUKURU MKOA WA TANGA KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI HADI SEPTEMBA 2020

**TANGA - OKTOBA 15, 2020**

## TAKUKURU MKOA WA TANGA YAOKOA FEDHA TASLIMU KIASI CHA SHILINGI 214,760,327.00 ZA SERIKALI PAMOJA NA WANANCHI

**Ndugu Wanahabari**

Habari za asubuhi

Nimewaita hapa leo ili nizungumze na wananchi wa Mkoa wa Tanga na Tanzania kwa ujumla kupitia ninyi wanahabari kwa lengo la kuujulisha umma juu ya utekelezaji wa majukumu ya Taasisi ya Kuzuia na kupambana na Rushwa Mkoa wa Tanga kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2020.

Huu ni utaratibu ambao Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa tumejiwekea ili Watanzania waweze kufahamu hatua mbali mbali zinazochukuliwa na TAKUKURU katika kutekeleza jukumu la Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini.

**Ndugu Wanahabari**

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii ya kipekee ya kukutana nanyi siku ya leo katika Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Tanga, karibuni sana.

Kwa Ujumla na kwa Ufupi nitazungumzia kazi zilizofanywa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa – TAKUKURU Mkoa wa Tanga kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2020 na pia mikakati yetu katika kipindi cha Oktoba – Disemba 2020 ikiwemo kuelekea kipindi hiki cha uchaguzi mkuu, utakaofanyika tarehe 28 Oktoba, 2020. Tunafanya hivyo pia ili kutekeleza matakwa ya Katiba, kwa maana ya kuwapa wananchi fursa na haki yao ya kupewa taarifa kuhusu matukio mbalimbali nchini, kama ilivyoelezwa katika ibara ya 18 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake.

**Ndugu Wanahabari**

Nianze na jukumu letu TAKUKURU la kuelimisha Umma;

Kwa mujibu wa kifungu cha 7(b) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007, TAKUKURU inalo jukumu la kuhimiza na kuendeleza uungaji mkono wa jamii katika kupambana na vitendo vya rushwa. Jukumu hili hutekelezwa kupitia Dawati la Elimu kwa Umma. Katika kipindi cha Julai hadi Septemba, 2020 TAKUKURU Mkoa wa Tanga tumeelimisha umma kwa kuendesha semina **77,** mikutano ya hadhara **78,** Ufunguzi wa Klabu mpya **15** za wapinga rushwa na Uimarishaji klabu **71** za wapinga rushwa zilizopo katika shule na taasisi mbalimbali mkoani Tanga, sambamba na kuandaa Habari na Makala **08**.

TAKUKURU Mkoa wa Tanga pia tumefanya vipindi vya redio **24** kupitia vituo vya redio vilivyopo mkoani Tanga lakini pia kutoa taarifa tano (**5**) kwa umma kupitia vyombo vya habari vilivyopo Mkoani Tanga na nitumie fursa hii kuwashukuru walimiki wa vyombo hivyo pamoja na wafanyakazi wao wote kwa kuwa sehemu ya kufanikisha hilo kwani mmekuwa mkiitika kila tulipo waita, Ahsanteni sana. TAKUKURU Mkoa wa Tanga tunahamasisha na kutoa elimu ya mapambano dhidi ya tukiamini kwamba wananchi wakiwa na uelewa kuhusu rushwa watachukua hatua ya kutoa taarifa, kukemea na kushirikiana na Serikali kwa hali na mali katika mapambano Dhidi ya Rushwa.

**Ndugu Wanahabari**

**Kuhusiana na Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na udhibiti.** Katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba 2020, TAKUKURU Mkoa wa Tanga Kupitia Mfumo wa Ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za Serikali, imefanya ufuatiliaji wa miradi **17** ya maendeleo katika Wilaya mbalimbali za Mkoa wa Tanga yenye thamani ya jumla ya Shilingi Bilioni kumi na mbili milioni mia nne themanini na tatu lakini sita sabini elfu na shilingi 42 na senti sabini na mbili tu (**Shilingi 12,483,670,042.72/=).** Miradi iliyofuatiliwa ni katika sekta za ujenzi, barabara, Elimu na maji. Sambamba na miradi ya Maendeleo TAKUKURU Mkoa wa Tanga pia imefanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za Serikali zinazotengwa kwa matumizi mbalimbali katika ofisi za Serikali na Taasisi za umma. Ufuatiliaji huu hufanyika kwa kufuatilia mtiririko wa fedha kutoka chanzo (Hazina, Wafadhili au Vyanzo vya ndani) mpaka mahali fedha zilipolengwa kutumika. Aidha ndani ya miezi mitatu umefanyika uchambuzi wa mifumo **10**, warsha **3** na ufuatiliaji wa maazimio **2** Mkoani Tanga.

**Ndugu Wanahabari**

**Dawati la Sheria na Mashtaka;**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 7(e) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 7 ya mwaka 2007, ni jukumu la TAKUKURU kuchunguza/ kupeleleza, na kwa maelekezo ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), kuendesha kesi mahakamani kwa kuwashitaki watuhumiwa wote wanaotuhumiwa kutenda makosa chini ya sheria hii na makosa mengine yanayohusisha Rushwa.

Katika Kutekeleza jukumu hili, ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Tanga tumepokea jumla ya taarifa **268** za vitendo vya Rushwa kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2020, Mchanganuo wa taarifa hizo kiidara unaonyesha kwamba Idara ya Afya **3,** Utawala **10**, fedha **8,** ujenzi **12,** Madini **5**, Misitu **9**, Mifugo 5, biashara 3, Halmashauri za Wilaya na Miji **27**, Mahakama **24**, Elimu **23**, Mirathi **16**, Kilimo **2,** Michezo **1**. Idara zingine zilizolalamikiwa ni pamoja na Magereza **1**, na Jeshi la Polisi **11,** Vyama vya ushirika **8**, SACCOS 2, VICOBA 4, NGO 1, Taasisi za Dini 1, Vyama vya Siasa **9,** Mashirika ya Hifadhi ya Jamii **16**, Tanesco 2, Uhamiaji **2,** TANROADS **3** na taarifa zinazohusu watu binafsi 33.

Aidha, baada ya kuzifanyia uchunguzi wa awali taarifa tajwa, taarifa **159** ziligundulika kwa ni za vitendo vya rushwa na taarifa **109** hazikuwa zinahusiana na vitendo vya Rushwa. Jumla ya taarifa **80** zimefungwa baada ya watoa taarifa kushauriwa na baadhi kuelekezwa kwenda Idara husika na taarifa **188** zinaendelea kuchunguzwa.

Kwa upande wa uendeshaji mashitaka TAKUKURU Mkoa wa Tanga kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba 2020, imeendesha jumla mashauri **16**

Mahakamani ambapo mashauri 13 yalifunguliwa kabla ya Julai 2020 na mashauri **03** ni kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba 2020.

Aidha kati ya kesi hizo **16** zilizoendeshwa mahakamani kesi **05** zilitolewa hukumu ambapo watuhumiwa **05** walikutwa na hatia na watuhumiwa wa kesi mbili waliachiwa huru kama ifuatavyo: Kesi yenye Na. Corr. Case 2/2019 Watuhumiwa wamehukumiwa kila mmoja kulipa faini ya Shilingi 1,000,000/= au kifungo cha mwaka mmoja jela na kwamba wamelipa faini kukwepa kifungu. Kesi Na. CC. 49/2019- mtuhumiwa alihukumiwa kwa makosa tisa kulipa faini ya Shilingi 6,000,000/= au kifungo cha miaka 10 jela ambapo mtuhumiwa alilipa faini na kukwepa kifungu. Pia kesi Na. CC 25/2018- ambapo mshtakiwa amelipa faini ya Shilingi 200,000/=. Katika kesi Na. ECC. 17/2018- watuhumiwa walikuwa 03 wawili waliachiwa huru na mmoja alitiwa hatiani hata hivyo aliyetiwa hatiani ni mrehemu. Aidha, katika kesi Na. CC 04/2018 watuhumiwa waliachiwa huru baada ya kuonekana hawana kesi ya kujibu na kesi Na. CC 05/2018 pia watuhumiwa waliachiwa huru.

**Ndugu Wanahabari**

TAKUKURU Mkoa wa Tanga katika kipindi hicho cha Julai – Septemba, 2020 imeweza kuokoa jumla ya **Shilingi 214,760,327.00** ambazo ni za Serikali pamoja na wananchi. Kwa Upande wa fedha zilizookolewa kutokana na kazi za uchunguzi na udhibiti, Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Tanga Katika Kuzuia na kupambana na rushwa, tumefanikiwa kuokoa fedha taslimu Shilingi milioni mia moja kumi na saba, laki saba elfu kumi na nne na mia tatu sabini na nne (Shilingi 117,714,374/=) zilizotokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa dhidi ya miamala ambayo haikuwa rafiki kwa mujibu wa Sheria, kanuni na taratibu mbali mbali. Pia ofisi imedhibiti kiasi cha Shilingi milioni tisini na saba arobaini

na tano na mia tisa hamsini na tatu (Shilingi 97,045,953/=) kiasi ambacho ni fedha za wananchi zilizofanyiwa ubadhilifu na hatimaye kiasi hicho kurejeshwa kwa wananchi.

**Ndugu Wanahabari**

TAKUKURU Mkoa wa Tanga tumejiwekea mikakati ya kupunguza na kumaliza kero kwa wananchi hasa katika maeneo yanayoongoza kwa kulalamikiwa kuwa na vitendo vya rushwa. Mikakati hiyo ni pamoja na;

a) Kuendelea kutoa Elimu kwa Umma katika makundi mbalimbali kuhusu athari mbalimbali za rushwa katika uchumi wa taifa letu na njia za kupambana na vitendo vya rushwa hususani katika kipindi hiki cha Uchaguzi Mkuu wa Rais na Wabunge.
b) Kuendelea na udhibiti kwa kuchambua mifumo mbalimbali ili kubaini mianya ya rushwa na kushauri jinsi ya kuziba mianya hiyo kwa lengo au nia ya kudhiti rushwa kwenye mifumo husika.
c) Kuendelea na kazi ya kufanya uchunguzi wa malalamiko ya vitendo vya rushwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa mapambano dhidi ya rushwa ili kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria kutegemeana na ushahidi unaopatikana.
d) Kuendelea Kuwahamasisha wananchi kutoa ushirikiano hasa inapohitajika wao kutoa ushahidi dhidi ya watuhumiwa wanapofikishwa mahakamani.
e) Kufuatilia matumizi ya fedha za Serikali, hususani katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, fedha za uboreshaji wa Elimu bure, kufuatilia na kuhakiki kodi zinazopaswa kulipwa Serikalini, Maabara na maeneo mengine yahusuyo utekelezaji wa sera mbalimbali kwa lengo la kuokoa

fedha za umma ili zitumike katika mambo yenye tija kwa wananchi wa Mkoa wa Tanga.

f) Kushirikisha Wadau katika mapambano dhidi ya rushwa ikiwa ni sambamba na kutoa taarifa mbalimbali kwa umma ili kukidhi matakwa ya sheria mbalimbali na pia kufikia uhalisia wa shabaha ya TAKUKURU ya kufanya kazi pamoja na wadau wote katika mapambano dhidi ya rushwa na kuifanya kuwa jambo hatarishi na lisilo na manufaa kwa njia ya kuelimisha, kuzuia, kubaini na kuwafikisha watuhumiwa wote mahakamani.

**Ndugu Wanahabari**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Tanga, tuna waomba na kuwahimiza wadau na wananchi kwa ujumla, kushiriki kwa namna mbalimbali katika mapambano dhidi ya rushwa hususani kipindi hiki cha Uchaguzi Mkuu. Nichukue pia fursa hii kuwasihi wananchi wote wa Mkoa wa Tanga kuendelea kuunga mkono mapambano dhidi ya rushwa ili kwa pamoja tuweze kufanikisha azma ya Serikali ya awamu ya tano ya kuhakikisha kwamba viongozi waadilifu ndio wanapewa dhamana ya kuongoza kwa ridhaa ya wapiga kura. Kwa kufanya hivyo tutafikia lengo la kupunguza vitendo vya rushwa katika jamii na hatimaye kuvitokomeza kabisa kwani Tanzania bila Rushwa inawezekana iwapo tutachagua viongozi wasiotoa rushwa. Natoa pia wito na ninawakaribisheni wananchi wote wenye Taarifa za vitendo vya rushwa kwenye ofisi za TAKUKURU Mkoa wa Tanga. Kwa wananchi waishio katika Jiji la Tanga wanaweza kutembelea ofisi yetu iliyopo eneo la Bombo karibu na Harbours Club, na kwa wale waishio Wilayani wasisite kufika katika ofisi za TAKUKURU zilizopo katika kila Makao Makuu ya Wilaya zote za Mkoa wa Tanga.

Aidha mwananchi au mdau yeyote anaweza kuwa siliana moja kwa moja na viongozi wa TAKUKURU Mkoa wa Tanga kwa namba zifuatazo:-

0689-797-998 na 0738-150-225(Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Tanga)
0784-280-663 na 0738-150-228 (Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Kilindi)
0782-208-008 na 0738-150-232 (Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Muheza)
0784-290-117 na 0738-150-230 (Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Lushoto)
0786-207-311 na 0738-150-233 (Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Pangani)
0782-866-867 na 0738-150-231(Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Mkinga)
0713-442-425 na 0738-150-229 (Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Korogwe)
0688-313-853 na 0738-150-227 (Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Handeni)

Pia wanaweza kupiga simu ya Bure 113 au kutuma ujumbe mfupi wa maandishi kwa kupiga *113# na kufuata maelekezo na kisha kutuo ujumbe wako.

Asanteni sana kwa kunisikiliza

Imetolewa na:

Dkt. Sharifa O. Bungala

**KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M)**

**TANGA**